

# MADHARA YA MBOLEA SANISI (CHUMVI CHUMVI) KWA

# LISHE



**M**bolea sanisi zina madhara ya muda mrefu kwa lishe/virutubisho. Kusudi lao pekee ni kuongeza mavuno kwa wakulima, lakini ongezeko la mavuno haliongezi ubora wa lishe ya chakula kilichozalishwa.

Katika Afrika, mbolea sanisi zinalenga zaidi kwenye mahindi na mpunga, kupitia ruzuku na mipango ya wafadhili. Hii imepelekea kupungua kwa bioanuai ya kilimo na anuai ya vyakula – vyote ambavyo ni muhimu kwa watu kuwa na afya.

Wakulima wanahitaji kuotesha mimea na mazao mengi ili kuwa na milo ya aina mbalimbali yenye lishe. Hii ni maalum hasa kwa nchi zinazoendelea, ambapo mara nyingi milo inakuwa na wanga zaidi na virutubisho vichache – kama vile vinavyotokana na wanyama, matunda, mbogamboga, maharage na jamii ya kunde. Aina mbalimbali za mazao pia yatamsaidia mkulima kuendelea kubaki na mfumo imara wa aina mbalimbali za mbegu, hasa katika hali za ukame na mabadiliko ya tabia nchi.